
Falsafa za Majuha
J.P MAKULA

J.P Makula
+255 765 711 520, johnmakula850@gmail.com
Arusha, Tanzania

Sanifu Kurasa
DL Bookstore
+255 787 163 013, dlbookstore@zoho.com
www.dlbookstore.com
Arusha, Tanzania

Sanifu Jalada
DL Bookstore
+255 787 163 013, dlbookstore@zoho.com
www.dlbookstore.com
Arusha, Tanzania

Chapa ya Kwanza 2022
© J.P Makula

ISBN 978 9987 789 32 0

HAKI ZOTE ZIMEHIFADHIWA
Haki zote zimehifadhiwa. Hairuhusiwi kunakili, kurudufisha, au kukitoa kielektroniki au kutumia sehemu ya kitabu hiki bila idhini ya mwandishi au mchapishaji. Kufanya hivyo ni uvunjifu wa sheria ya haki miliki.

*Hii ni hadithi ya kubuni.*
*Haimhusu mtu yeyote aliye hai wala aliyekufa. Endapo jina au tukio fulani litafanana na jambo lililowahi kutukia, linalotukia ama litakalotukia, jambo hilo lichukuliwe kama sadfa tu, na kuwa halikukusudiwa na mwandishi.*
*Kwa sababu, hii ni HADITHI YA KUBUNI.*

*Natabaruku riwaya hii kwa wazazi wangu (Gasper Makula &*
*Regina Makala*
*ambaye amekuwa na mchango mkubwa sana,*
*katika uandishi wangu.*

# 3

*KWENDA MWANAKWENDA.*

Hekaheka za nusu saa iliyopita zilinifanya nisionane na mjomba Masele. Baada ya kikao kifupi cha wanafamilia na baada ya kuweka mwili pale uwanjani nilipata fursa ya kuzungumza na mjomba japo kwa ufupi.

"Pole kwa safari na msiba mjomba." Alinipa pole baada ya kusalimiana.

"Asante sana mjomba… poleni pia."

"Tutapoa, ni vigumu kuamini ila hatuna budi kulipokea jambo hili." Nilitikisa kichwa kukubaliana naye. Baada ya mazungumzo nilikaa kwenye mstari pamoja na wanakijiji nikiwa nimefuatana na shemeji yangu, yeye mbele, mimi nyuma. Nilisogelea jeneza nikiwa na mchanganyiko wa hisia,

kwanza shauku ya kujiridhisha kwa mara nyingine kama kweli mwamba umedondoka, pili hofu ya kukabiliana na kifo na tatu kukata tamaa ya maisha na mzigo wa mawazo juu ya hatima ya mwanadamu hapa ulimwenguni. Tulikuwa tukisogea mmoja baada ya mwingine. Huyu anatamani kufika aliyefika anajuta! Safari ya hatua chache pale uwanjani ilionekana ndefu na ya kuchosha pengine kuzidi hata safari ya Dar es salaam. Baada ya safari ya dakika kadhaa za kuburura miguu kuelekea kaskazini hatimaye tulifika. Alianza yeye kwani alikuwa mbele yangu, hakukawia kama waombolezaji wengine, alichungulia kwa sekunde chache tu majuto yakampiga ngwara akadondoka chini kama gunia. Akina mama waliwahi pale mara moja wakambeba wanguwangu wakatokomea nae upande wa mashariki kuelekea Nzega.

Ni yeye; nilifika nikahakikisha. Ukiacha rangi yake kukolea kuuthibitishia umma wa waombolezaji kwamba alikuwa mwafrika halisi, hakubadilika sana. Ni kama alikuwa kwenye usingizi mzito baada ya siku nyingi za kukesha akijiandaa na mitihani. Wangeniruhusu nimtolee pamba walizokuwa wamemwekea puani na kumpepea angepata pumzi yake iliyopotea. Wangeniruhusu nimtolee pamba walizokuwa wamezizika masikioni mwake angesikia sauti ya kilio chetu akaamka. Wangedhani nimechanganyikiwa, pagawa, mwendawazimu. Nilisimama pale kumtazama niduwae hadi uchungu usambae katika kila kiungo cha mwili wangu. Hakuna hata kiungo kimoja kilichosahaulika. Ulifika miguuni kulegeza misuli yake nishindwe kutembea. Ukapanda juu kukeketa tumbo, nikashiba. Ukaendelea na safari mpaka kifuani kuziba mirija ya hewa nikose pumzi. Ukapondaponda sakafu ya moyo wangu iliyokuwa imesalia na kuweka kigingi kwenye mirija usiweze kusukuma damu,

almanusura niage dunia. Ukapanda kukaba koo langu nikashindwa kumeza. Domo langu pia lilitiwa kufuli, nikashindwa kusema. Siku hiyo ndipo akili yangu ilipofungwa nikawa juha, kilaza, zumbukuku. Mwishowe ulitoboa macho, nikayaona maruerue. Yakatoka machozi kusafisha mboni za macho yangu, nikayafuta nimwone mjomba Masele akija kunipa bega nichechemee kuondoka pale, huenda ningesimama milele yote!

Baada ya kujiridhisha kwamba kila aliyekuwa na shauku ya kuona ameona, mjomba alifunika jeneza. Waliopata mikono ya kubebea jeneza walishirikiana kubeba jeneza hadi kaburini. Mimi na waombolezaji wengine tulijivuta pole pole nyuma yao. Kwa kuwa Padri aliyesalisha misa asubuhi alirejea Nzega mjini mchana na asingeweza kufika kuendana na mabadiliko ya ratiba ya mazishi wakati ule, matumaini yalihamia kwa katekista ambaye kwa bahati mbaya pia alikuwa amesafiri kwenda kwenye kongamano huko mkoani Mwanza. Waombolezaji wengi walionekana kuhuzunishwa na kukosekana kwa watumishi wa Mungu katika mazishi ya mpendwa wetu lakini mimi sikuona ulazima wa mwafrika kuzikwa kwa miongozo ya kirumi, kingereza, kijerumani, kimarekani au kiarabu, cha msingi ni kuweka mwili kwenye shimo na kuweka udongo juu yake; shughuli ambayo tumeifanya karne nyingi zilizopita kabla ya ujio wa hivi visasili kutoka ughaibuni.

Nikiri wazi kwamba sikuwahi kuwa katili na msaliti kabla ya siku ile. Alianza mama, akifuatiwa na ndugu wengine na ilipofika zamu ya jamaa niliinua mikono nikachota udongo nikautupa shimoni kuisaidia ardhi kummeza swahiba wangu! Inahuzunisha lakini hicho ndicho kilichotakiwa kufanyika wakati ule. Wanakijiji waliendelea kutupa udongo shimoni

kwa kupokezana hadi shimo lilipojaa. Waliweka udongo uliozidi katika umbo la mstatili. *Nsumba ntale* aliongoza utaratibu wa kuweka shada juu ya kaburi. Baada ya ndugu mimi pia nilipata fursa ya kuweka ua juu ya kaburi, kwa wakati huo tuliweka kama ishara ya upendo kwa mpendwa wetu lakini sasa naona ni kama tulikuwa tukimpa zawadi kwa kupenda upeo. Wakati tukiendelea kuweka shada kwenye kaburi fahamu zilimrejea shemeji yangu, akiwa ameshikiliwa na mama mmoja apataye miaka arobaini aliweka shada pia. Kabla ya zoezi kutamatika alitokea binti mmoja mnene kiasi, maji ya kunde rangi yake, sura nzuri ya kwake, tukimpa masika nne atatosha kuwa mke wa mtu lakini alionekana bado anakwea vidato. Alipokwisha kuweka shada kisha kufagia machozi kwa kiganja cha mkono wake wa kuume, kwa uchungu alisikika akisema.

"Kwenda mwanakwenda… kwenda usigeuke. Kwenda ukitabasamu, kwenda marehemu. Ulikuwa mwema lakini dunia imekuwa katili kwako. Ulipenda upeo ila kifo ndiyo ruwaza ya mapenzi yako. Kifo chako ni ushahidi tosha kwamba dunia haikukustahili. Tuache na mahangaiko ya dunia ya wafu wanaoishi, pata haki huko uendako. Kwenda usigeuke…kwenda… kwenda mwanakwenda." Baada ya kutamka maneno yale aligeuka akapita katikati ya kundi kubwa la waombolezaji, akaenda zake. Mkono wa kuume wa kaburi la baba yake tulimpumzisha. Jioni ile Mwamba na jua vilizama kwa pamoja, kukawa giza, kimya.

Yalipotimia yale yaliyotabiriwa na wahenga kwamba kila nafsi iliyopata kuishi kwa shida na raha ionje umauti na kuyaficha yaliyotokea kwenye shimo, tulilala sio fofofo hadi jua lilipouzidi mwezi kwa miale yake. Nilinawa uso kuondoa tongotongo machoni nilione vizuri kaburi nitoneshe donda

ndugu lililokwisha kupona moyoni mwangu. Nilikunja ngumi, nikakita konde upande wa kushoto wa kifua changu, nikapata ahueni. Tukaagana na wenyeji wetu kisha tukaianza safari ya kurejea Dar es Salaam, ukiwa!